Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

## Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania

*Dar es Salaam,*
*12 Februari, 2026.*

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUISHA LESENI ZA UFANYAJI BIASHARA YA BIMA

1. Sheria ya Bima Sura ya 394, imeipa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) jukumu la kusimamia shughuli zote za bima nchini ikiwemo kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma za bima kwa lengo la kuhakikisha uimara, ustahimilivu wa sekta ya bima na kulinda haki za wateja wa bima.

2. Kwa kuzingatia sheria hiyo watoa huduma za bima wote zikiwemo kampuni za bima wanatakiwa kuhuisha leseni za biashara kila mwaka ili kuwapa uhalali wa kuendelea kufanya biashara ya bima nchini.

3. TIRA inapenda kuutaarifu Umma kuwa watoa huduma ambao leseni zao hazijahuishwa hawana uhalali wa kufanya shughuli za bima ikiwemo kuandikisha au kuchukua biashara mpya za bima, kutoa au kuhuisha hati za bima (insurance policies renewals), kutangaza au kufanya matangazo ya biashara ya bima na kufanya shughuli za uwakala, ushauri wa bima na nyinginezo.

4. Hivyo, Umma unahimizwa kuhakiki uhalali wa leseni za kampuni za bima au mtoa huduma za bima kabla ya kufanya muamala wowote wa biashara ya bima kwa kuangalia orodha ya kampuni za bima au watoa huduma za bima wenye leseni halali kupitia tovuti ya TIRA ambayo ni www.tira.go.tz au kuhakiki taarifa za kampuni au watoa huduma za bima kupitia TIRAMIS APP kwa kuingiza namba ya usajili iliyotolewa na TIRA au fika Ofisi ya TIRA iliyo karibu nawe.

5. Vilevile, watoa huduma za bima wanahimizwa kuhuisha leseni zao ili kuendelea kuwa na uhalali wa kufanya biashara ya bima na endapo kuna mtoa huduma yeyote mwenye changamoto awasiliane na TIRA. Aidha, Wananchi mnaombwa kutoa taarifa endapo mtabaini uwepo wa Watoa huduma za bima wasio na leseni.

   TIRA, Kwa Soko Salama la Bima.

**Imetolewa na**
**MENEJA UHUSIANO NA MAWASILIANO KWA UMMA**
**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA (TIRA)**

Makao Makuu ya TIRA, Jengo la TIRA BIMA HOUSE,
Barabara ya TIRA, Njedengwa, S. L. P. 2987, Dodoma – Tanzania | Simu: +255 (026) 232 1180 Nukushi: +255 (026) 232 1180
Barua pepe: coi@tira.go.tz, Tovuti: www.tira.go.tz